UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA (TCAA), DKT. JABIRI K. BAKARI, KUELEKEA MKUTANO WA SABA WA DUNIA WA USAFIRI WA ANGA WA SHIRIKA LA KIMATAIFA LA USAFIRI WA ANGA (ICAO), TAREHE 16–20 NOVEMBA 2026, MONTRÉAL, CANADA



Dkt. Jabiri K. Bakari
Mkurugenzi Mkuu

Salamu!

Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga linatarajia kufanya Mkutano wa Saba wa Dunia wa Usafiri wa Anga (ICAO ATConf/7), kuanzia tarehe 16 hadi 20 Novemba 2026 jijini Montréal, Canada.

Mkutano huu unafanyika katika kipindi muhimu kwa upande wa usafiri wa anga wa kimataifa. Sekta ya usafiri wa anga ikiendelea kushuhudia mabadiliko makubwa yanayochochewa na ongezeko la mahitaji ya soko la usafiri wa anga, kukuwa kwa maendeleo ya teknolojia, mabadiliko ya mwenendo wa soko, pamoja na hitaji linaloongezeka la uwekezaji endelevu katika miundombinu.

Mkutano huu, unaobeba kaulimbiu isemayo “Usafiri wa Anga: Kichocheo cha Kuunganisha Dunia, Maendeleo ya Kiuchumi na Ustahimilivu katika Ulimwengu Unaobadilika,” ni fursa muhimu kwa Nchi Wanachama, Mamlaka za udhibiti na wadau wa sekta kutafakari mustakabali wa usafiri wa anga wa kimataifa na kuimarisha ushirikiano katika kujenga mfumo wa usafiri wa anga duniani wenye ufanisi, stahimilivu, jumuishi na endelevu.

Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, usafiri wa anga unaendelea kuwa kichocheo cha kimkakati katika maendeleo ya kiuchumi, mtangamano wa kikanda, utalii, biashara na uwekezaji. Ikizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kuendelea kujenga sekta ya usafiri wa anga iliyo salama, yenye ulinzi madhubuti, ufanisi na ushindani ni muhimu katika kuimarisha muunganiko wa nchi yetu na kuiweka Tanzania kuwa lango la kimkakati la usafiri wa anga barani Afrika na kwingineko.

Sekta ya usafiri wa anga nchini Tanzania imeonesha ukuaji mkubwa katika kipindi cha miaka kumi na mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa Takwimu za Usafiri wa Anga Tanzania za mwaka 2012 na mwaka 2025, idadi ya abiria imeongezeka kwa takriban asilimia 100, kutoka abiria milioni 4.06 mnamo mwaka 2012 hadi abiria milioni 8.11 mnamo mwaka 2025. Katika kipindi hicho hicho, miruko ya ndege imeongezeka kutoka 222,430 hadi 297,285, sawa na ongezeko la asilimia 34, huku shehena ya mizigo kwa njia ya anga ikiongezeka kutoka tani 32,411 hadi tani 44,076, sawa na ongezeko la asilimia 36.

Ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya sekta ya usafiri wa anga, TCAA inaendelea kuimarisha mifumo yake ya usimamizi na ya kitaasisi. Imefanya mapitio na kuuishaKanuni za Usafiri wa Anga mwaka 2026, pamoja na maboresho ya kisheria yanayolenga kuimarisha usimamizi wa usalama wa usafiri wa anga, hii ikiwa ni ishara ya dhamira ya Mamlaka ya kudumisha mfumo wa kisasa wa udhibiti unaoendana na viwango vya kimataifa na mahitaji mapya ya sekta.

Mamlaka inaendelea kutoa kipaumbele kwa usimamizi wa usalama na ulinzi wa usafiri wa anga, uboreshaji wa huduma za kisasa za uongozaji ndege, mageuzi ya kidijitali katika michakato ya usimamizi, pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi. TCAA inaendelea kuwekeza katika kuendeleza wataalamu wa usafiri wa anga na kuimarisha uwezo wa kutoa mafunzo, ikiwemo kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC). Juhudi hizi ni muhimu katika kujenga ujuzi wa kitaalamu na kiufundi unaohitajika ili kuhimili hali ya ki mazingira ya usafiri wa anga inayozidi kuleta changamoto mpya.

Vilevile, TCAA inatambua fursa zinazotokana na hatua za kufungua soko la usafiri wa anga kwa awamu, hususan kupitia Soko Moja la Usafiri wa Anga Afrika (SAATM). Kupanuka kwa fursa za kuingia katika masoko na kuimarika kwa muunganiko wa kikanda kunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika biashara, utalii, uwekezaji na mtangamano wa kiuchumi. Hata hivyo, manufaa ya kufungua soko lazima yaambatane na usimamizi madhubuti wa usimamizi, uwezo wa kutosha wa kitaasisi, na uzingatiaji endelevu wa viwango vya kimataifa vya usalama na ulinzi wa usafiri wa anga.

Wakati jumuiya ya kimataifa ya usafiri wa anga ikitafakari mbinu mpya za udhibiti wa kiuchumi, ugharamiaji wa miundombinu, ubunifu na ustahimilivu wa sekta, TCAA inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa maboresho ya ki usimimazi yanatekelezeka, jumuishi, na yanayozingatia uwezo na mahitaji tmbalimbali ya maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga.

Kwa msingi huo, Mkutano wa Saba wa Dunia wa Usafiri wa Anga ni jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu, kubaini changamoto za pamoja za udhibiti, na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa kuelekea maendeleo endelevu ya usafiri wa anga.

TCAA inaendelea kujizatiti kushirikiana kwa karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ICAO, mashirika ya kikanda ya usafiri wa anga, wadau wa sekta na washirika wa maendeleo ili kujenga mazingira wezeshi ya usimamizi yanayovutia uwekezaji, yanayoimarisha muunganiko, na yanayohakikisha kuwa usafiri wa anga unaendelea kuchangia kwa tija katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Taifa.

Kupitia usimamizi madhubuti, ubunifu na ushirikiano wa kimataifa, tunaweza kujenga sekta ya usafiri wa anga iliyo salama, yenye ulinzi madhubuti, stahimilivu, shindani, na iliyo tayari kutumia fursa na kukabili changamoto za siku zijazo.